

Dhoruba Inajikusanya

Ripoti ya kukabiliana na pengo la uzalishaji wa gesi chafu ya mwaka wa 2021



Wakati dunia inapoweka juhudi za kupunguza uzalishaji wa gesi chafu - juhudi ambazo bado hazitoshi - toleo la sita la *Ripoti ya UNEP ya kukabiliana na pengo la uzalishaji wa gesi chafu: Dhoruba Inajikusanya* inaonyesha kuwa ongezeko la madhara kwa mazingira yanaendelea kwa kasi sana kuliko juhudi zetu za kukabiliana na hali hiyo.

Ulimwengu unahitaji kuimarisha juhudi za kukabiliana na athari zisizoweza kugeuzika za mabadiliko ya tabianchi.

- Ahadi za sasa chini ya Mkataba wa Paris zinaonyesha kutakuwa na ongezeko la joto la nyuzijoto 2.7 duniani kufikia mwishoni mwa karne hii.
- Kukabiliana na gesi chafu kunaweza kupunguza madhara kwa mazingira yanayoongezeka kwa kasi joto linapoongezeka. Hata hivyo, hatari kwa mazingira bado zipo, na gharama za kukabiliana nazo huongezeka athari kwa mazingira zinapoongezeka.
- Ijapokuwa upunguzaji mkuu ndio njia mwafaka zaidi ya kupunguza athari na gharama za mda mrefu, kuimarisha ahadi za kukabiliana na hali ni muhimu ili kuzuia mapengo yaliyopo kuongezeka.

Kukabiliana na pengo kunazidi kujumuishwa kwenye sera na mikakati kote ulimwenguni.

- Asilimia 79 ya nchi zimepitisha angalau mkakati mmoja wa kitaifa kukabiliana na gesi chafu (mpango, mkakati, sera au sheria) - ongezeko la asilimia 7 tangu mwaka wa 2020.
- Asilimia 9 ya nchi ambazo hazina mkakati wa aina hii zimeanza kuweka.
- Takribanj asilimia 65 ya nchi zina mkakati mmoja au zaidi wa kisekta.

Utekelezaji wa hatua za kukabiliana na gesi chafu unaongezeka polepole kote ulimwenguni.

- Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo linaonyesha kuwa wafadhili kumi wakuu walifadhili zaidi ya miradi 2,600 inayolenga kukabiliana na uzalishaji wa gesi chafu kati ya mwaka wa 2010 na mwaka wa 2019.
- Miradi inazidi kuimarika, huku mingi ikivutia ufadhili zaidi ya dola za Marekani milioni 10.
- Kiwango duni cha mifumo ya ufuatilaji na tathmini ni cha kusikitisha: ni asilimia 26 tu ya nchi zina mfumo kama huo. Hata hivyo, asilimia 36 ya nchi nyinginezo zinaunda mfumo.

Lakini fedha zinazohitajika kutekeleza mipango ya kukabiliana na gesi chafu hazitoshi.

- Gharama za kukabiliana na gesi chafu huenda zikaongezeka na kukadiriwa kufikia dola za Marekani kati ya bilioni 140 na bilioni 300 kwa mwaka kufikia mwaka wa 2030 na dola za Marekani kati ya bilioni 280 na bilioni 500 kwa mwaka kufikia mwaka wa 2050 kwa nchi zinazoendelea pekee.
- Ufadhalii wa mazingira unaofanywa katika nchi zinazoendelea ili kuweka na kutekeleza mikakati ya kukabiliana na gesi chafu zilifikia dola za Marekani bilioni 79.6 katika mwaka wa 2019.
- Makadirio ya gharama za kukabiliana na gesi chafu katika nchi zinazoendelea ni kubwa mara tano hadi kumi zaidi kuliko mtiririko wa sasa wa fedha za umma za kukabiliana na gesi chafu. Pengo la ufadhili wa kukabiliana na uzalishaji wa gesi chafu inaongezeka.
- Fursa ya kutumia hela za kuijimarisha baada ya janga la COVID-19 kufadhili mikakati na utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na gesi chafu inapotea (tazama makala kuhusu jinsi janga la COVID-19 linavyoathiri juhudzi za kukabiliana na uzalishaji wa gesi chafu).

Licha ya mafanikio fulani, juhudzi zaidi zinahitajika za kufadhili na kuwezesha utekelezaji.

- Dunia inapaswa kuimarisha ufadhili wa umma za kukabiliana na gesi chafu, kupitia uwekezaji wa moja kwa moja na kukabiliana na vikwazo vyta kukabiliana na hali katika sekta za binafsi.
- Utekelezaji wa hatua dhabiti zaidi za kukabiliana na gesi chafu unahitajika ili kuepuka kushindwa kudhibiti madhara kwa mazingira, hasa katika nchi zinazoendelea.
- Ulimwengu pia unahitaji kuzingatia majanga mabaya kabisa kwa mazingira yanayoangaziwa na Ripoti ya Sita ya Tathmini ya Jopo la Kimataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi katika juhudzi zake za kimataifa za kuimarisha ufadhili wa kukabiliana na gesi chafu utekelezaji wa mikakati.